

# Malezi nchini Australia

## Parenting in Australia

Swahili/Kiswahili

**Wazazi kutoka jamii na tamaduni zote wanachangia upendo wa watoto wao na wanawatachia kila la kheri. Kuna njia nyingi za kuwakuza watoto. Baadhi ya njia zinazotumika kulelea watoto hapa Australia zinaweza kuwa mpya kwako.**

Malezi katika utamaduni mpya

Ukiwa ni mzazi katika mazingira mapya unaweza kugundua kwamba:

- > maisha ya watoto wako ni tofauti na yale uliyokuwa nayo ulipokuwa kijana
- > badhi ya vitu vinavyotarajiwa kutoka kwa wazazi siyo vile ulivoyovizoea
- > familia yako inayotegemewa ni finyu kuliko zamani.

Kama una jambo unataka kumweleza mtu, au una wasiwasi au kuna shida kuna watu wengi na huduma mbalimbali zinazoweza kukusaidia. Itakuwa vizuri kama utatambua haupo peke yako.

**Wazazi wana umuhimu mkubwa kuwasaidia watoto wao kuzoea nchi mpya. Huwafundisha maadili ya familia na wanaweza kuwasaidia kujifunza, kufikia malengo, na kuendelea kukumbatia utamaduni wao.**



Kila mmoja katika familia anazoea maisha katika utamaduni mpya. Kushirikiana kutafuta suruhu kunaweza kuimarisha familia.

## Sheria inasemaje kuhusu malezi

Sheria ya Australia huruhusu wazazi kuwalea watoto katika tamaduni na imani zao ili mradi watoto wako salama na wanaangaliwa vizuri.

Wazazi wanahitaji kuhakikisha kwamba watoto:

- > wako salama na hawadhusuri
- > wanapata sehemu safi ya kuishi, chakula na mavazi
- > wanaenda shule
- > wanapata matibabu
- > wanasaidiwa kiuchumi.

Wazazi wana wajibu kwa watoto wao mpaka watakafikia miaka 18. Wakifikisha miaka 18 na zaidi, watoto kisheria huwa ni watu wazima. Wengi huendelea kuishi katika familia zao.

Haijalishi aina  
ya familia uliyonayo,  
ndicho kitu muhimu  
kuliko vyote katika  
maisha yawatoto.

## Familia katika Australia

Kuna aina nyingi za familia katika Australia.

Familia ambazo zina:

- > mama, baba na watoto
- > mzazi mmoja anayelea watoto
- > wazazi waliotengana au kutalikiana ambao wanachangia malezi
- > watu wazima na watoto kutoka ndoa zilizopita wanaoishi kama familia moja
- > wazazi wa jinsia moja - wanawake 2 au wanaume 2 na watoto wao
- > mababu na mabibi au watu wazima wanaokuza watoto.

Baadhi ya familia ni ndogo. Baadhi zina watoto wengi au ndugu wengi wakishi pamoja.





## Njia za malezi

Kuna njia nydingi za kukuza watoto. Wazazi wa Kiaustralia wanatakiwa wafanye yafuatayo:

- > kuwa wema na wenyewe subira
- > kutumia muda kuwa na watoto, wakicheza, wakiongea na kuburudika
- > kuwaongoza watoto na kuwasaidia kujifunza
- > kuelewa wanavyohisi watoto
- > kuwa na sheria za kifamilia zilizo wazi na zinazoleweka
- > kutafuta msaada pale penye wasiwasi.

Akinababa nao wanahimizwa:

- > kuhusika katika malezi ya watoto tangu siku wanapozaliwa
- > kumuheshimu mama watoto na wanawake wote katika familia
- > kuwalinda watoto dhidi ya vurugu katika familia.

**Kulea kunakuwa rahisi pale ambapo watu wazima katika familia wanashirikiana kukuza watoto.**

Wazazi ni muhimu pia. Jaribu kupumzika pale unapoweza, fanya vitu unavyovifurahia, na uwe makini na afya yako.

## Kuwa na mahusiano mazuri na watoto

Kuwa na mahusiano mazuri na watoto wako hufanya malezi kuwa rahisi. Baadhi ya njia za kujenga mahusiano mazuri ni:

- > kuzungumza na kuwasikiliza watoto wako
- > kula chakula pamoja kama familia
- > kugawana kazi za nyumbani
- > sherehekeea mafanikio
- > tatua matatizo kwa pamoja
- > kuwa na makubaliano ya pamoja kuhusu sheria za kifamilia, kama kuwa mwema na mwangalifu, kutokupigana, kupiga kelele au kubandikwa majina; kusema ‘samahani’, kupeana nafasi na kutumia muda sawa; kuangalia TV au kutumia simu au skrini nydingine.



Mahusiano huwa imara pale watoto wanapohisi kusikilizwa.

## Mawazo kuhusu kujifunza kwa watoto

Kuna namna nyingi wazazi wanaweza kuwasaidia watoto wao kujifunza. Unaweza:

- > kuwahadithia vitabu tangu utotoni - katika Kiingereza au lugha nyingine au kuwasimulia hadithi kutoka kwenye utamaduni wako
- > kuwahamasisha kuchezea vitu vingi na wawe wakakamavu nje
- > kuwafundisha watoto kufanya vitu wenywewe
- > kuonesha furaha wanapojifunza kitu kipyä.

**Watoto hufaidika wanapojiunga na vituo vya kulelea watoto, vikundi vya michezo na shule za awali tangu wakiwa na umri mdogo. Watoto wenyewe ulemavu wanakaribishwa katika huduma hizi namashueni. Watoto wote wana haki ya kupata elimu.**




## Vipi kuhusu tabia?

Wazazi wanahamasishwa kuwa wapole na wakarimu pale watoto wanapojifunza tabia wanayoitarajia.

Hili linaweza kusaidia:

- > kueleza kile unachokitaka na umuhimu wake
- > kuwapa watoto muda kufanya mazazoezi ya tabia hiyo
- > kujaribu kuelewa chanzo kilichopelekea 'tabia mbaya'
- > kuwa mpole, hata kama unahisi hasira
- > kuzungumza na watoto na kutoa mapendekezo ya pamoja.

**Kuwapiga au kuwafokea watoto hakuwasaidii kujifunza. Wanaweza kutii ila watakosa nafasi ya kujifunza kutatua matatizo. Adhabu kali za kimwili kwa watoto ni kinyume cha sheria. Kuna huduma mbalimbali zinazoweza kusaidia pale unapoendelea kuwa na changamoto.**



Watoto hujifunza kutokana na kile waonachokifanya wazazi. Daima uwe na ile tabia unayotaka mtoto wako awe nayo.

## Watoto wanaweza kuchukuliwa mbali na wazazi?

Baadhi ya wazazi wana wasiwasi kwamba watoto wao wanaweza kuchukuliwa.

- > Hii ni nadra sana.
- > Inatokea pale ambapo watoto wanakuwa kwenye hatari ya ukatili, unyanyasaji au kupuuzwa.
- > Mashirika yanasaidia familia kutatua matatizo na kuwatunza watoto salama. Ni vizuri kupata msaada mapema kabla ya mambo kuharibika.

## Vurugu katika familia

Vurugu katika familia ni tatizo katika jamii na tamaduni zote. Kamwe vizuri. Inamdhuru kila mmoja katika familia.

- > Msongo wa mawazo huathiri watoto hata kama hawajaona au kusikia vurugu. Watoto walioko tumboni wanaweza kuathirika pia.
- > Watoto hawawezi kujifunza vizuri au kufikia mambo mazuri ambayo wazazi wanawataki.
- > Vurugu katika familia inafanya watu wazima washindwe kuwatunza watoto.

**Kama unatumia vurugu au una matatizo ya hasira, kuna mashirika ambayo yanaweza kusaidia.**

Vurugu katika familia ni kinyume na sheria za Australia.

## Haki na wajibu

Wakati mwingine watoto hufikilia kama wana 'haki' zaidi nchini Australia. Wazazi wanaweza kuwasaidia kuelewa kuwa 'haki' zozote zinakuja na majukumu, yakiwemo:

- > kuonyesha heshima kwa wanafamilia na wengineo
- > kutii sheria
- > kujitunza na kuwatunza wengine salama.

**Kama watoto watazungumzia 'haki' zao nchini Australia, unaweza tafuta ukweli kwa kutumia ushauri wa kisheria mtandaoni au huduma nyingine. Unaweza kuomba mkalimani.**

## Kupata msada

Ni sawa kuomba msaada pale unapohitajika. Kuna huduma ambazo zinaweza kuwasaidia wazazi kujua zaidi kuhusu kuwalea watoto au kukabiliana na dukuduku lolote ndani ya familia. Madaktari, mashule na mashirika mengine mwishoni mwa Muongozo huu ni mahala pazuri pa kuanzia.

# Huduma

## Dharura

000 Polisi, Moto, Gari la wagojwa (Police, Fire, Ambulance)  
13 14 44 Kuita Polisi kama kuna tatizo lakini ikiwa siyo hatari ya haraka

## Wakalimani

### Kituo cha Ukalimani na Tafsiri ya Lugha (Interpreting and Translating Centre)

1800 280 203, saa 2.30 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Wakalimani kwa njia ya simu au wa ana kwa ana [www.translate.sa.gov.au](http://www.translate.sa.gov.au)

### Huduma ya Ukalimani na Tafsiri (Translating and Interpreting Service (TIS National))

13 14 50 muda wowote mchana au usiku kwa wakalimani wa kwenye simu [www.tisnational.gov.au](http://www.tisnational.gov.au)

## Malezi

### Simu kwa ajili ya Usaидizi wa Malezi (Parent Helpline)

1300 364 100 kwa ushauri kuhusu afya ya mtoto na malezi

### Islamicare – Simu kwa ajili ya Usaидizi wa Malezi (Islamicare – Parenting Helpline)

1800 960 009, siku 7 kwa wiki  
Msaada wa siri kwa wazazi wa vijana <http://Islamicare.org.au>

### Mtandao wa Malezi ya Watoto (Raising Children Network)

Taarifa kuhusu malezi pamoja na video katika lugha nyingi  
<http://raisingchildren.net.au>

### Malezi SA (Parenting SA)

Miongozo mingine miepesi kwa wazazi pamoja na miongozo mingine ya kawaida kuhusu mada mbalimbali, ikiwa ni pamoja na 'Kuwa mzazi', 'Je, ni mtindo gani wa malezi unaoutumia?' [www.parenting.sa.gov.au](http://parenting.sa.gov.au)

## Afya na ustawi

### Huduma ya Afya ya Wakimbizi (Refugee Health Service)

8237 3900 au 1800 635 566 (wanaoita kutoka vijiji) saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
21 Market Street, Adelaide  
Huduma ya afya kwa wakimbizi wapya na wanaotafuta hifadhi

### Healthdirect

1800 022 222 wakati wowote mchana au usiku ikiwa mtu anaumwa au amejeruhiwa [www.healthdirect.gov.au](http://www.healthdirect.gov.au)

### Huduma ya Taifa ya Madaktari wa Nyumbani (National Home Doctor Service)

13 74 25 kuomba daktari wa baada ya saa za kazi akutembelee nyumbani <https://homedoctor.com.au>

### Huduma ya Afya kwa Watoto na Familia (Child and Family Health Service (CaFHS))

1300 733 606, saa 3 asubuhi-saa 10.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa ili kufanya miadi  
Huduma ya bure kwa watoto wachanga na watoto wadogo wenye umri kati ya miaka 0-5. Wauguzi wanaweza kukusaidia kuhusu afya ya watoto, kula, kulala na ukuaji  
Angalia [www.cyh.com](http://www.cyh.com) kwa maelezo kuhusu afya ya watoto na malezi

### Huduma ya Afya ya Akili ya Watoto na Vijana (Child and Adolescent Mental Health Service (CAMHS))

8161 7198 au 1800 819 089 (wanaoita kutoka vijiji) saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Huduma ya ushauri wa bure kwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-15 [www.wch.sa.gov.au/camhs](http://www.wch.sa.gov.au/camhs)

### Mahusiano Australia (Huduma kwa tamaduni mbalimbali) (Relationships Australia)

1300 364 277 au 1800 182 325 (wanaoita kutoka vijiji) saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Msaada kuhusu mahusiano ya kifamilia, watoto na vijana, kamari, vurugu, VWU, ugojwa wa maini [www.rasa.org.au](http://www.rasa.org.au)

## Elimu

### Idara ya Elimu (Department for Education)

Tafuta pale unapoishi huduma za serikali zeny, vituo vya watoto, chekechea au shule [www.education.sa.gov.au](http://www.education.sa.gov.au)

### Kundi la Michezo SA (Playgroup SA)

Tafuta kundi la michezo lililo karibu yako [www.playgroupsa.com.au](http://www.playgroupsa.com.au)

### Serikali ya Australia (Australian Government)

Maelezo juu ya huduma ya watoto na shule ya awali. Tafuta kituo chako cha mahali unapoishi [www.mychild.gov.au](http://www.mychild.gov.au)

## Sheria

### Tume ya Kutoa Huduma za Kisheria SA (Legal Services Commission of SA)

Simu kwa ushauri 1300 366 424, saa 3 asubuhi-saa 10.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Ushauri wa bure wa kisheria [www.lsc.sa.gov.au](http://www.lsc.sa.gov.au)

## Huduma za Tamaduni Mbalimbali

### Shirikisho la Wanawake wa Kiafrika SA (African Women's Federation of SA)

8161 3331 au 8354 2951, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu, Jumatano, Alhamisi  
304 Henley Beach Road, Underdale  
Mipango na huduma kwa wanawake wa Kiafrika [www.awfosa.com](http://www.awfosa.com)

### AMES Australia

7224 8550, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Sakafuni, 212 Pirie Street, Adelaide  
7224 8500, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
2/59 Commercial Road, Salisbury  
Huduma za makazi kwa wakimbizi na wahamiaji wapya [www.ames.net.au/locations/find-sites](http://www.ames.net.au/locations/find-sites)

### Kituo cha Vitendeakazi cha Wahamiaji Australia (Australian Migrant Resource Centre)

8217 9500, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
23 Coglin Street, Adelaide  
Makazi, mahusiano ya kifamilia pamoja na huduma kuhusu unyanyasaji wa kifamilia kwa wahamiaji, wakimbizi na wanaotafuta hifadhi Angalia [www.amrc.org.au](http://www.amrc.org.au) kwa maeneo ya mijini na vijiji

### Shirika la Wakimbizi Australia (Australian Refugee Association)

8354 2951, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
304 Henley Beach Road, Underdale  
8281 2052, saa 3.30 asubuhi-saa 10.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
1 Brown Terrace, Salisbury  
Usimamizi na usaizidi kwa wakimbizi [www.australianrefugee.org](http://australianrefugee.org)

### Vijana wa Tamaduni Mbalimbali SA (Multicultural Youth SA (MYSA))

8212 0085, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Shop 9 Miller's Arcade, 28 Hindley Street, Adelaide  
Mipango kwa vijana na familia [www.mysa.com.au](http://www.mysa.com.au)

### Shirika la Wanawake wa Kiislam SA (Muslim Women's Association of SA)

8212 0800, saa 3.30 asubuhi-saa 9 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Ghorofa ya 4, 182 Victoria Square, Adelaide  
Mipango na msaada kwa wanawake wa Kiislam na familia zao [www.mwasa.org.au](http://www.mwasa.org.au)

## Vurugu katika Familia

### Simu kuhusu Vurugu za Majumbani (Domestic Violence Crisis Line)

1800 800 098 muda wowote mchana au usiku  
Msaada kuhusu vurugu, malazi ya dharura na uhamisho <http://womenssafetyservices.com.au>

### Mpango wa Kusaidia Wanawake Wahamiaji (Migrant Women's Support Program)

8152 9260, saa 2.30 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Msaada wa siri na wa bure kwa wanawake na watoto wahamiaji walio kwenye unyanyasaji wa kifamilia <http://womenssafetyservices.com.au>

### 1800 RESPECT

1800 737 732 muda wowote mchana au usiku  
Zungumza na mtu kwa simu au kwenye mtandao kuhusu unyanyasaji familia au ubakaji [www.1800respect.org.au](http://1800respect.org.au)

Mwongozo huu rahisi wa Mzazi ni mmoja kati ya 9 iliyoundwa na Parenting SA kwa ajili ya familia kutoka kwenye jumuiya mpya zeny tamaduni mbalimbali na zinazoendelea kujitokeza Australia ya Kusini. Tungependa kushukuru mashirika mengi pamoja na familia ambazo zimechangia bure maarifa na utaalam kwenye Miongozo, hasa familia na wafanyakazi ambao picha zao zinaonekana ndani yake.

Parenting SA inashirkiana na Idara ya Elimu na Mtandao wa Afya wa Wanawake na Watoto.

**Simu (08) 8303 1660**  
[www.parenting.sa.gov.au](http://www.parenting.sa.gov.au)

**Mwongozo Rahisi wa Wazazi unatolewa bure Australia ya Kusini**

**Muhimu:** Taarifa hii haikusidii kuchukua nafasi ya ushauri kutoka kwa mtaalamu.

© Serikali ya Australia ya Kusini Toleo la kwanza 01/2019.



Government  
of South Australia